


# Unapodhani wewe au mtoto wako anaugua malaria

Nampeleka Juma zahanati.  
Hali yake sio nzuri leo.



Katika zahanati hii, kwa sasa tunatumia kipimo hiki kipya cha malaria kiitwacho malaria Rapid Diagnostic Test kwa kifupi mRDT.



Ni kipimo kizuri sana.  
Nitachukua tone la damu ya Juma na kuipima kuona kama ana malaria.




## Hiki ndicho kipimo kipya cha malaria kinachoitwa kipimo cha haraka (mRDT).




Ndani ya dakika 20 kipimo kitatoa majibu sahihi chenyewe kuonesha kama kuna malaria.

Kipimo kimeonesha Juma ana malaria  
Hakikisha unampa kidonge kimoja asubuhi na kingine jioni kwa siku tatu.




Una maswali yoyote mama?



Asante.

Nimeelewa Juma anatakiwa kumaliza vidonge vyote vya malaria hata kama anaonekana kupata nafuu kwa sababu tunatakiwa kuua vimelea vyote.

## Wakati mwingine, mRDT itaonesha hamna malaria




**Joseph anajisikia ni mdhaifu na ana maumivu ya mwili. Anakwenda zahanati kupata ushauri.**

Joseph, kwanza nitapenda kukufanyia uchunguzi kisha nitakupima na kipimo cha mRDT.



**Majibu ya kipimo yameonesha Joseph hana malaria.**



Joseph, Kipimo kinaonesha hauna malaria.


Ni kipimo cha uhakika na kisipoona malaria inamaana hakika hakuna malaria.

## Wakati mwingine, mRDT itaonesha hamna malaria

Nadhani una vimelea vya maradhi kama mafua. Unatakiwa kumeza paracetamol na kupumzika.

Hauna haja ya kumeza dawa za malaria kwa sababu mRDT inaonesha hauna malaria.

Kama una swali lolote nitafurahi ikiwa utaniuliza.



**Akiwa nyumbani, Joseph alimeza paracetamol na kunywa maji. Na pia alipumzika.**

Joseph hakumeza dawa za malaria kwa sababu mRDT ilionesha hakuwa na malaria.



**.....siku chache baadaye.**




Kwa sasa nimepata nafuu.

Mhudumu wa afya alikuwa sahihi, sihitajiki kumeza dawa za malaria ikiwa kipimo cha malaria kinaonesha sina malaria.

## Waambie majirani na familia yako.

Mambo Joseph.  
Umepona?



Poa, Nashukuru ninaendelea vizuri.

Katika zahanati walitumia kipimo  
kipya cha Malaria kinachoitwa mRDT

Kipimo hicho kilionesha sina malaria.

Mhudumu wa afya akanielezea kuwa  
dawa za malaria hazitanisaidia.

Akanishauri nipumzike na kumeza  
paracetamol. Sasa sijambo.

### Tumia kipeperushi hiki kuwaelezea wanajamii kuhusu kipimo cha mRDT.

Njia pekee kujua kama sisi au watoto  
wetu wana malaria ni kupima.

Kwa sasa katika zahanati kuna kipimo  
kipya kizuri cha malaria kinachoitwa  
mRDT.

Nilipimwa sikuwa na malaria.

Mhudumu wa afya alinieleza kuwa  
sasa hivi malaria inapungua, hivyo  
tutarajie majibu yasiyoonesha malaria  
zaidi katika eneo letu.



Tunafurahi kuwa watu wachache zaidi  
wanaugua malaria siku hizi.

Sasa tunaamini ushauri wa wahudumu  
wanapopima malaria.

